OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MTIHANI WA KIDATO CHA NNE JARIBIO LA 04
KISWAHILI

MUDA: SAA 3

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina Sehemu A, B na C zenye jumla ya Maswali Kumi na Moja (11)
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, na B na MawIli (02) kutoka Sehemu C.
3. Sehemu A ina alama kumi na sita**(16),** Sehemu B ina alama hamsini na nne**(54)** na Sehemu C ina alama thelathini (30)
4. Zingatia maelekezo ya kila Sehemu na kila swali
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyo ruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kitabu chako cha kujibia

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali yote

1.Chagua herufi ya ibu sahihi katika sehemu uliyoppewa

i) Amina ni mwimbaji wa mahsairi kila akiimba mashairi yake mshororo wa mwisho katika kila beti zake haubadiliki katika kila beti zote anapoimba, mshororo huo usiobadilika tunaweza kuupa jina gani, kati ya haya kishairi?

a) Mshororo takriri
b) Mshororo uradidi
c) Bahari
d) Kituo bahari
e) Kituo

ii) Neno cheza ni kitenzi kikuu na kitenzi kikuu huunda kishazi huru, na kishazi tegemezi vile vile, huundwa na kitenzi ila utofauti wake ni kwamba.

a) Kishazi tegemezi huundwa na vishazi vyenye viambishi vya o-rejeshi
b) Kishazi tegemezi huundwa na sehemu ya karifu inayokaliwa na kielezi
c) Kishazi tegemezi huundwa na vitenzi vyenye viambishi vilivyorejeshwa
d) Kishazi tegemezi huundwa na sehemu ya kiarifu inayokaliwa na Nomino
e) Kishazi tegemezi ni mada ya sarufi tegemezi

iii) Mende anapenda kula uchafu. Neno uchafu lililopigwa mstari lipo katika ngeli ipi?

a) KI-VI
b) I- ZI
c) YU/A-WA
d) KU
e) LI-YA

iv) Mtangazaji, wa kituo cha habari cha TBC hukakikisha watazamaji wake wanapata habari sahihi kwa wakati katika kazi ya fasihi hiyo hufanywa na nani kati ya hawa wafuatao?

a) Wasikilizaji
b) Wazungumzaji
c) Hadhira
d) Fanani
e) Wasomaji

v) Rais Samia hupenda sana kutumia methali na nahau katika hotuba mbali mbali seti zifuatazo ni methali isipokua moja ni nahau. Je ni ipi?

a) Asiye na mwana aeleke jiwe
b) Aliye juu mngoje chini

c) Amemranda mma yake
d) Alioye mbali haangukiwe na mti
e) Asiye na hili na lile

vi) Ni jambo gani linadhihirisha upekee wa kazi ya kifasihi?

a) Muundo wa kazi husika
b) Wahusika wa kazi husika
c) Jina la kazi husika
d) Jina la mtunzi wa kazi husika
e) Mtindo wa kazi husika.

vii) Jolini na Nasra walifanikiwa kuwa “Watamfitinia” mwalimu wao kwa mkuu wa shule yao. Je, azimio hilo la Jolini na Nasra katika kauli ipi kati ya zifuatazo?

a) Kutenda
b) Kutendana
c) Kutendea
d) Kutendeana
e) Kutendewa

viii) Rahma aliandika habari kuhusu nchi ya Tanzania katika habari hiyo alizingatia mpangilio mzuri na unaoeleweka kwa wasomaji wa habari yake, je kwa uelewa wako alichokizingatia Rahma kinajulikana kama nini?

a) Mantiki
b) Insha
c) Wazo
d) Ayaaa
e) Kistari

ix) “Said ameoa”, “Juma ameoa”na “Shabani kaoa”katika utoaji wa sauti kipi ni sahihi kuzingatia hizo tungo tatu hapo juu?

a) Mkazo
b) Lafudhi
c) Kiimbo
d) Matamshi
e) Alama za uandishi

x) Ashura alifurahi alipopata mawswali yote ya Kiswahili. Neno lililopigiwa mstari ni.

a) Nomino
b) Kielezi

c) Kitenzi
d) Mofimu
e) Kishazi

2. Oanisha maelezo ya dhana yaliyo katika orodha A kwa kuchagua herufi ya dhana husika katika Orodha B. Kisha andika herufi husika katika karatasi ya majibu.

ORODHA A	ORODHA B
i) Lugha ya kibantu	A. Kumbukumbu za mkutano
ii) Katambuga, kifaru na nyau	B. Akronimia
iii) Uambatanishaji	C. Habari leo
iv) Gazeti la utawala wa kiingereza	D. Habari za leo
v) Muhtasari wa mambo muhimu yanayojadiliwa na kukubaliana katika mkutano	E. Ufananisho F. Nyungumawe G. Kiswahili
vi) Humtofautisha na wasanii wengine wa jamii yake	H. Mtindo I. Muundo

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. Bainisha mzizi wa asili wa kila neno katika maneno yafuatayo;

i) Mkimbizi
ii) Maji
iii) Waligawana
iv) Muumbaji
v) Nisingelipenda

b) Upatanisho wa kisarufi ni kigezo kimojawapo kati ya vigezo vya kuunda ngeli za nomino. Thibitisha dai hili kwa kutunga sentensi mbili katika kila ngeli kwenye ngeli;

i) Ngeli ya pili
ii) Ngeli ya tatu
iii) Ngeli ya nne
iv) Ngeli ya tano

4. Vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi ni kama sarafu ya shilingi ambayo haiwezi kugawanyika. Taja vipengele vitano vya fani na vipengele vine vya maudhui

5. Idadi ya sentensi za Kiswahili ni sawa na idadi ya mafiga ya jiko. Kwa kutumia mifano taja nakuzitolea maana zake.

6. Lucy alimwambia mwanamke kuwa katika ulimwngu huu, kila kitu kinachimbuko na asili yake. Kiswahili kina sili yake kinadharia"kwa mifano madhubuti, thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne.

7. (a) Nini maana ya semi
(b) Semi zina vipera vyake. Fafanua vipera vitano na kutoa mfano mmoja kwa kila kipera.

8. (a) Fafanua maana ya misimu kama ilivyofasiriwa katika lugha ya Kiswahili.
(b) Msimu ina sifa nyingi katika lugha ya Kiswahili. Taja sifa tano za misimu katika lugha.

SEHEMU C (Alama 40)

Jibu maswali mawili (02) katika sehemu hii

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

Wasakatonge	-	M.S.Khatibu
Malenga Wapya	-	TAKILUKI
Mshairi ya Chekacheka	-	T.A Mvungi

RIWAYA

Takadini	-	Ben. J. Hanson
Watoto wa Manantilie	-	E. Mbogo
Joka la Mdimu	-	A. J. Safari

TAMTHILIYA

Orodha	-	Steve Raynolds
Ngoswe Penzi Kitovu ch uzembe	-	E. Semzaba
Kilio chetu	-	Medical aid foundations

9. Mwanachama huweza kupata changamoto mbali mbali katika maisha yake ya kila siku. Kwa kutumuia riwaya mbili kati ya ulizozisoma. Fafanua kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya.

10. Chagua mashairi matatu kwa kila diwani kutoka kati ya diwani mbili ulizosoma kisha onyesha jinsi washairi walivyo walimu bora kwa jamii ya leo.

11. Kutokukubaliana miongoni mwa jamii kumekuwa chanzo cha mivutano mbli mbali kati yao na kupelekea kukosekana na kwa amani, utulivu na utengamano katika jamii. Onehsa ukweli wa kauli hii kwa kufafanua mivutano iliyoibuliwa na waandishi wa tamthiliya ulizosoma kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu.